# Uhusiano Wetu na Mungu

[Our Relationship with God – Swahili]    [2nd Edition – September 2013]


| | | Ukurasa |
|---|---|---|
| Somo la 1 | Ukuu wa Mungu | 1 |
| Somo la 2 | Mungu alimwumba mtu kwa mfano wake | 5 |
| Somo la 3 | Dhambi ni nini? | 9 |
| Somo la 4 | Matokeo ya dhambi | 12 |
| Somo la 5 | Mungu anafanya njia | 16 |
| Somo la 6 | Yesu yu hai | 19 |
| Somo la 7 | Kitu gani lazima tufanye | 23 |
| Somo la 8 | Sisi ni viumbe vipya | 27 |



Mwandishi:

Erling Rasmussen
John Ronaldson
Ivor Lewis

**SBCI, P.O. Box 324, Hillcrest 3650, South Africa**
**E-mail: admin@sbci.co.za    Tel. 0873510934**
**www.sbci.co.za**



**Nakili © 1998 All Africa Bible College**
**Kitabu hiki kinalindwa na sheria za kunakili za kimataifa. Ina ruhusiwa kunakili kitabu chote au sehemu ya kitabu kwa maandishi ya mkono au kukichapisha kwa kutumia mashine. Ujumbe usibadilishwe kwa namna yoyote ile; wala kitabu au nakala ya kitabu isiuzwe kwa ajili ya kujipatia kipato. Ruhusa hii ina tolewa na All Africa Bible College ambao itambuliwe kuwa ndio watoaji wa kitabu na kibali cha mafundisho haya.**

# Ukuu wa Mungu

**Soma la 1**

## A. Utangulizi

Kabla hatujaongelea kuhusu kumjia Mungu, lazima tujue yeye ni nani. Katika somo hili tutajaribu kutoa muhtasari wa utukufu na ukuu wa Mungu.

Biblia inatuambia kuna njia tatu anazotumia Mungu kwa kutusaidia kuelewa jinsi alivyo wa ajabu.

**1.** Mungu amejifunua kwetu katika uumbaji wake unaotuzunguka. Warumi 1:20.

**2.** Mungu amejifunua kwetu kwa neno lake. Yohana 1:1.

**3.** Mungu aliufunua utukufu wake kwetu kwa njia ya mwanawe pekee Yesu Kristo Waebrania 1:1-2; Yohana 1:18.

## B. Maono ya utukufu wa Mungu

**Soma Isaya 6:1-7**

Mungu alimpa Isaya maono ya ukuu wake wa ajabu ambayo imeandikwa kwenye Biblia kwa ajili yetu.

**1.** Aya ya 3. Makerubi walikuwa wakilia na kusema “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu”, wakimsifu Mungu daima bila kuchoka na kusujudia mbele zake.

Tunapokuwa katika uwepo wake, wajibu wetu ni – kumsifu Yeye – kwa kuwa yeye ni mtakatifu na mkuu sana.

**2.** Aya ya 5. Matokea ya kusimama kwa Isaya mbele za Mungu ilimfanya aseme, “Ole wangu”. Alijitambua kuwa yeye hakuwa safi na wala hakustahili kusimama mbele za mwenyezi Mungu.

**3.** Aya ya 8. Mwishowe, Isaya alilia akisema, "Nipo hapa unitume mimi". Kujifunua kwake Mungu kulimpa Isaya hamu ya kumtumikia Mungu.

Tunahitaji ufunuo wa kujua Mungu ni nani. Ufunuo wake kwetu kutatufanya tumwabudu Yeye, kutembea naye na kumtumikia Yeye.

## C. Mungu ni mkamilifu

**Soma Zaburi 90:1-2**

Mungu alikuwepo wakati wote, na wala hakuumbwa na yeyote. Kulikuwa na wakati ambapo Mungu Baba, Mwanawe Yesu Kristo na Roho Mtakatifu walikuwepo peke yao tu.

**1.** Hakukuwepo na Malaika wa kuziimba sifa zake.

**2.** Hakukuwa na nyota, jua au mwezi katika anga ili kuuonyesha utukufu wake. Ulikuwepo utupu tu.

**3.** Dunia na milima yake pamoja na bahari haikuwepo.

Hii haikuwa kwa siku moja, mwezi au mwaka, bali tokea milele na milele.

Ukweli wa ajabu ni kwamba Mungu hakuhitaji kuwa na viumbe vyake ndipo awe na furaha.

Mungu alikuwa na **furaha** tele kama alivyo hata leo.
Alikuwa na **amani** tele kama alivyo hata leo.
Alikuwa **upendo** kama alivyo hata leo.
Alikuwa mtakatifu **kikamilifu** kama alivyo hata leo.

Mungu katika Utatu wake, yaani Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, aliufurahia Uungu wake mwenyewe. Hakuhitaji kitu chochote kwa ajili ya kumfurahisha.

## D. Tabia kuu za Mungu

Mungu anazo sifa nne ambazo hakuna mwingine awaye yote aliye nazo.

**1. Anajua kila kitu.**

**Soma Warumi 11:33-34**

a) Hii inamaanisha kwamba anajua vitu vyote – vilivyopita, vilivyopo na vijavyo.

b) Mungu ana hekima zote. Hakuna kitu asichokijua. Hii ni pamoja na vitu vyote ambavyo ni halisi na vile vinavyowezekana. Paulo na Isaya kwa pamoja waliuona ufunuo huu wa Mungu.

c) Aya ya 33. Utajiri wa hekima na ufahamu wa Mungu una kina kisichopimika. Kwa sababu hii hukumu za Mungu ni kamilifu na hazipingiki.

d) Kifungu cha 34. Sisi, kama wanadamu, hatuwezi kupima njia zake.

Je, Mungu alimwendea nani kwa ushauri? Hakuna awezaye kumshauri Mungu. Yeye anajua vyote.

**2. Yupo kila mahali.**

**Soma Zaburi 139:7-13**

a) Hii inamaanisha kwamba Mungu yupo kila mahali kwa wakati mmoja. Mungu hafungwi na sheria za nyakati na za mahali.

b) Daudi alistaajabishwa alipofahamu kuwa Mungu yupo kila mahali kwa wakati mmoja. Kama angelipaa hadi mbinguni, au angelishuka hadi kilindi ya kina

kirefu, Mungu yupo pale. Na kama angelikwenda mahali popote hapa duniani, Mungu yupo.

Ni faraja ya ajabu kwetu kufahamu kwamb popote tuendapo au chochote kinachotupata, Mungu yupo kwa ajili yetu.

**3. Mungu ni Mwenyezi.**

**Soma Mithali 30:4**

a) Mwenyezi inamaanisha kwamba Mungu ni mwenye uwezo wote.

b) Mungu alipoziumba mbingu na nchi, alitamka neno tu na mbingu nanchi zikafanyika. Waebrania 11:3.

c) Je, uwezo wake utalinganishwa na nini?

d) Ni jambo kubwa kufahamu kwamba Mungu huzungumza nasi na kwamba hutupatia nguvu tunapomtazama Yeye.

Kama Yeremia tunatakiwa kutangaza, "Aa, Bwana Mwenyezi ... Hakuna jambo gumu kwako". Yeremia 32:17.

**4. Habadiliki.**

**Soma Waebrania 13:8**

a) Hii inamaanisha kwamba Mungu habadiliki wakati wowote.

b) Mungu ni Mungu yule yule kabla ya uumbaji, na Yeye ndiye Mungu wa Agano la Kale na Agano Jipya, naye atabakia hivyo milele.

Kila kitu duniani kitatoweka lakini Mungu atabakia alivyo. Waebrania 1:10-12.

c) Wengine wanaweza kutufedhehesha lakini Mungu hawezi kututahayarisha. Siku zote twaweza kutegemea ahadi za Mungu. Hesabu 23:19.

## E. Mungu yu juu ya viumbe vyake vyote

**Soma 1 Mambo ya Nyakati 29:11**

**1.** Katika mstari wa mwisho wa sala ya Bwana Yesu alituambia tusali hivyo. Mathayo 6:13b.

**2.** Kila siku tunahitaji kukumbushwa juu ya ukuu wa Mungu wetu. Jinsi alivyo wa utukufu na ukuu. Yeye ni mkuu kuliko kitu chochote katika viumbe vyake vyote. Kwa kweli, utukufu wote ni wake.

## Aya ya kukumbuka

Kutoka 15:11, *"Ni nani kati ya miungu aliye kama wewe ee Bwana? Ni nani kama wewe-mkuu katika utakatifu, utukufu wa kutisha, na matendo ya ajabu?"*

## Muhtasari wa Mwalimu

**1.** Soma Ayubu 42:2, Zaburi 115:3 na uone jinsi Mungu wa maandiko alivyo, na daima atakuwa Mfalme wa wafalme, na Bwana wa mabwana.

**2.** Hebu fikiria majina ya Kiebrania alizopewa Mungu wetu, na uwashirikishe washirika wako. Wewe pia waweza kutumia majina haya katika mahubiri kwa kuelezea ukuu wa Mungu.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Yehovah | – | mmoja Wa Milele; Yeye aliyekuwa, aliyeko, na atakayekuja. | |
| Yehovah Elohim | – | muumbaji Wa Milele; aliye pekee. | Mwanzo 2:4-25. |
| Yehovah Adonai | – | Bwana mwenyezi wetu. | Mwanzo 15:2, 8. |
| Yehovah Jireh | – | Bwana atupaye mahitaji yetu. | Mwanzo 22:8, 14. |
| Yehovah Nissi | – | Bwana aliye Bango letu. | Kutoka 17:15. |
| Yehovah Ropheka | – | Bwana mponyaji wetu. | Kutoka 15:26. |
| Yehovah Shalom | – | Bwana amani yetu. | Waamuzi 6:24. |
| Yehovah Tsidkeenu | – | Bwana wa haki yetu. | Yeremiah 23:6. |
| Yehovah Mekaddishkem | – | Bwana atutakasaye. | Kutoka 31:13. |
| Yehovah Sabaoth | – | Bwana wa majeshi. | 1 Samweli 1:13. |
| Yehovah Shammah | – | Bwana yupo. | Zaburi 48:35. |
| Yehovah Elyon | – | Bwana aliye juu sana. | Zaburi 7:17. |
| Yehovah Rohi | – | Bwana, mchungaji wangu. | Zaburi 23:1. |
| Yehovah Hoseenu | – | Bwana muumba wetu. | Zaburi 95:6. |
| Yehovah Eloheenu | – | Bwana Mungu wetu. | Zaburi 99:5. |

# Mungu alimwumba mtu kwa mfano wake

**Soma la 2**

## A. Utangulizi

**Soma Isaya 43:7**

Katika somo lililopita tuliona jinsi Mungu alivyo katika utakatifu na nguvu zake. Katika Somo hili tutaona jinsi Mungu alivyoumba wanadamu kwa mfano wake, na jinsi tulivyoumbwa kiajabu.

**1.** Katika Isaya 43 Mungu asema kwamba tuliumbwa kwa ajili ya utukufu wake.

**2.** Tukijiangalia wenyewe kwa macho ya Kimungu, tutaona jinsi tulivyo wa thamani kwa Mungu na kwa watu.

## B. Uumbaji

**Soma Mwanzo 1:26-27, 2:7**

**1.** Mungu katika utatu wake – yaani Baba, Mwana na Roho Mtakatifu – walishauriana pamoja kumwumba mtu.

**2.** Mungu alituumba; wala hatukujiumba wenyewe. Zaburi 100:3.

**3.** Mungu hakusema nasi tuwe kama jua, mwezi, nyota na dunia, lakini kwa upendo alimfanya mtu kwa mikono yake mwenyewe. Zaburi 119:73.

**4.** Kisha akapulizia uhai ndani ya Adamu na akawa kiumbe hai.

## C. Aliumbwa kwa sura ya Mungu

**1.** Tunapoangalia duniani leo na kuona jinsi wanabamu wamvyoanguka katikatope la dhambi, inakuwa vigumu kuona kuwa tumeumbwa kwa mfano wa Mungu lakini Mungu hakukusudia iwe hivi.

**2.** Tunaposoma Biblia tunaona kwa njia nyingi jinsi tulivyofanana na Mungu.

a) **Kiroho** — Mungu alituvuvia asili yake ya kiroho ambayo hutufanya tuwe juu kuliko wanyama. Sisi peke yetu kati ya viumbe vyote vya nchi tuna ushirika na Mungu. Ayubu 32:8.

b) **Utu wetu** — Mungu ni nafsi. Yeye ni nafsi iliyo juu kulikoyote, mwenye **(nafsi)** uhuru wa kufanya atakalo. Mwanadamu pia alipewa uhuru wa kuchagua kati ya mema na mabaya.

c) **Utakatifu** — Mungu ni mtakatifu, na mwanadamu aliumbwa awe safi na mtakatifu kama ilivyo sura ya Mungu.

d) **Upendo** — Mungu ni pendo. Mtu aliumbwa ili ampende Mungu na wanadamu wenzake.

e) **Utawala** — Mungu ni Mwenyezi (Bwana wa wote) na aliumba mtu ili atawale vi umbe vyote.

f) **Sura ya** — Mtu ni mtoto wa Mungu, aliyeumbwa kwa sura yake, akiakisi Kimungu sura ya Kimungu kati ya wakazi wote wa nchi.

**3.** Sababu tumeumbwa kwa sura yake twaweza kumfahamu.

## D. Aliumbwa kiajabu

**Soma Zaburi 139:13-16**

Hebu tufikirie vitu vya kushangaza katika mwili wa mtu na kuona jinsi tulivyoumbwa kiajabu.

**1.** Tukiangalia mwili wetu tutaona kwamba hakuna watu wawili duniani waliofanana sura kabisa. Mungu aliumba kila mtu kwa namna yake. Kwa mfano, alama za dole gumba za mtu mmoja ni tofauti kabisa na ya mwenzake.

**2.** Moyo wetu ambao ni pampu iliyoko kifuani, haihitaji kuambiwa ifanye kazi aukuwashwa. Lakini husukuma damu mara 4200 kwa saa, yaani sawa na lita 12000 ya damu kwa kila siku.

**3.** Katika miili yetu tunayo misuli 600 na mishipa ya damu yenye urefu wa kilometa 1500. Katika masikio yetu tunayo vinyweleo 20000 inayosaidia kuchuja sauti mbali mbali zinazotuzunguka.

**4.** Hakuna kompyuta yoyote duniani inayoweza kusogelea uwezo wa ubongo wa binadamu.

Hizi ni baadhi tu ya vitu vya ajabu kuhusu mwili wetu.

Mungu hakumwumba mtu yeyote kuwa mkuu kuliko mwenzake. Matendo 10:34. Sisi sote tunaye Baba mmoja ambaye ni Mungu, tumetokana na baba wa kibinadamu mmoja, Adamu, na Mungu hana upendeleo kwa mtu.

## E. Thamani ya mtu

Watu wengi duniani hawajui jinsi walivyo wa muhimu kwa Mungu na jinsi Mungu anavyowathamini wanadamu. Kwa sababu ya kutoelewa jambo hili huuana wao kwa wao na kufanyiana vibaya kuliko wanyama. Lakini ona jinsi Mungu anavyotuona wa maana:

**1.** **Mamlaka.**

**Soma Zaburi 8:3-8**

Mungu alipowaumba Adamu na Hawa aliwapa kutawala viumbe vyote. Mwanzo 1:27-28.

**2.** **<u>Dhamani kubwa</u>.**

**Soma Marko 8:36**

Machoni pa Mungu mwanadamu ana thamani kubwa kuliko ulimwengu wote.

**3.** **<u>Gharama ya wokovu</u>..**

**Soma 1 Petro 1:18-19**

Gharama kubwa kuliko yote ililipwa kwa ajili ya wokovu wetu – uhai wa Mwana wa Mungu ulitolewa.

**4.** **<u>Umuhimu wa milele</u>.**

**Soma Yohana 11:26**

Kwa sababu Mungu alituvuvia uzima wake wa milele ndani mwetu, hatuwezi kufa, ila tutaishi milele na milele. Kwa hiyo, sisi ni watu wa muhimu sana sana.

**5.** **<u>Kufanana na Muumbaji</u>.**

**Soma Mwanzo 9:6**

Kwa sababu tumeumbwa kwa mfano wa Muumba na tumeinuliwa juu ya viumbe vyote, uhai wetu wa kibinadamu ni wakfu sana.

## F. Ushirika na Mungu

**Soma 1 Yohana 1:3**

**1.** Ilikuwa ni furaha ya Mungu kuwa na ushirika na mwanadamu tokea alipoumba mtu wa kwanza. Alitembea wakati wa jioni katika Bustani ya Edeni ili kuwa na ushirika na Adamu na Hawa.

**2.** Mungu huwa na mipango nasi hata kabla ya kutuumba tumboni mwa mama zetu. Jeremiah 1:5; Ayubu 31:15.

**3.** Mungu hutushika mikono yetu na kutuambia tusiwe na hofu, kama vile mtu anavyomshika mkono mtoto wake kumfariji wakati wa hatari. Isaya 41:13.

**4.** Tutakuwa na ushirika wa milele na Mungu na tutatawala milele naye. Tutafanya kazi pamoja na Mungu tukiyaongoza mambo yasiyo na mwisho. Ufunuo 5:10, 22:4-5.

## G. Anguko kuu lenye msiba

**1.** Ulikuwa ni mpango wa Mungu kwetu tuvitawale viumbe vyake, tuongezeke na kubarikiwa naye.

**2.** Alimwumba Adamu akiwa hana dhambi, lakini pamoja na hayo alimpa uhuru wa kuchagua kutenda au kitotenda dhambi. Mungu alifanya agano na Adamu kwamba Adamu hatakufa endapo hatakula tunda la mti wa ujuzi wa mema na mabaya.

**3.** Shetani katika sura ya nyoka, alikuja na kumjaribu adamu. Adamu kwa makusudi alitenda dhambi na hivyo akauharibu uhusiano wake na Mungu.

**4.** Kwa sababu ya dhambi hii kubwa, mwanadamu na viumbe vyote walilaaniwa na Mungu na hakuweza tena kuwa na ushirika na Mungu.

Lakini Mungu ametufanya kwa sura yake na kwa utukufu Wake na anataka tuwe na ushirika sisi kwa sisi.

Katika masomo yafuatayo tutaona dhambi ni kitu gani rekebisho la Mungu kwa dhambi.

### Aya ya kukumbuka

Mwanzo 1:27, *"Mungu aliumba mtu kwa mfano wake, katika sura ya Mungu alimwumba, mwanaume na mwanamke aliwaumba"*.

### Muhtasari wa Mwalimu

**1.** Mtu aliumbwa kama Mungu kwa vile yeye ana sehemu tatu. 1 Wathesalonike 5:23.
Mtu ana **mwili** – nyama mifupa na sehemu tano za hisia kama vile kugusa, kunusa, kuonja,kuona na kusikia.
Anayo **nafsi** – huu ni ufahamu (nia), hisia (kujisikia), na utashi (uwezo wa kuamua mambo).
Anayo **roho** – inayowasiliana na Mungu, dhamira ya mtu inayomwonyesha mema na mabaya, ufahamu wake humwonyesha mapenzi ya Mungu.

**2.** Asili ya mwanadamu ya kimwili na ya kiroho imeonyeshwa wazi katika maandiko:
a) Mwili (wala siyo nafsi na roho) iliumbwa mavumbini. Mwanzo 2:7.
b) Roho hutengana na mwili kifoni. Yakobo 2:26; Luka 16:22.
c) Mwili (wala siyo nafsi) waweza kuuawa. Mathayo 10:28.
d) Roho hutamani, lakini mwili ni dhaifu. Mathayo 26:38-41.
e) Mwili pamoja na roho humtukuza Mungu. 1 Corinthians 6:20.
f) Mtu wa ndani ni wa milele, wakati mwili hufa. 2 Corintians 4:16-18.
g) Roho ya mtu yaweza kufa, wakati mwili wake unaishi. Waefeso 2:1.
h) Nafsi na roho za wenye haki huenda mbinguni wakati wa kifo (2 Wakorintho 5:8), na miili yao huenda kaburini. (Yohana 5:28-29).
i) Nafsi na roho za wenye dhambi huenda kuzimuni, wakati miili yao inapoenda kaburini. Luka 16:19-26.

# Dhambi ni nini?

**Somo la 3**

## A. Utangulizi

**Soma 1 Samweli 12:15**

Biblia yatuambia kwamba Mungu hapendezwi na dhambi na hivyo twahitaji kugeukia mbali na dhambi zetu. Katika somo hili tutaangalia kwa undani maana ya dhambi.

## B. Je, kwenye Biblia dhambi huitwaje?

1. **Dhambi ni uasi dhidi ya Mungu.**

   **Soma 1 Samweli 15:23**

   a) Shetani alijulikana mwanzoni kama Lusifa,mmoja wa malaika Mungu aliowaumba ili kumtukuza. Lusifa alijiinua juu kwa majivuno,akiiasi amri ya Mungu, na kwa hivyo akatupwa chini mpaka dunia, kutoka juu mbinguni.

   b) Mungu huchukulia uasi kuwa ni jambo baya sana. Mungu hufananisha uasi na uchawi na kuabudu sanamu.

   c) Roho ya shetani ya uasi dhidi ya Mungu inafanya kazi duniani hata leo, ikiwasukuma watu wayakatae mamlaka ya Mungu na kumvuta mtu kufuata njia zake mwenyewe.

   d) Watu wengi husema kwamba wao hawana dhambi. Wanaishi maisha mazuri. Hawaibi wala kuua na bado hawamwachii Mungu maisha yao, na kumtafuta kwa mioyo yao yote.

   Mungu alituumba sisi tuwe na uhusiano naye. Mungu ni lazima afanyike wa kwanza mioyoni mwetu. Maisha yetu yote ni lazima apewe Yeye wakati tunapotafuta kumpendendeza kwa njia ya imani.

2. **Dhambi iko katika matendo yetu.**

   **Soma 1 Yohana 3:4**

   a) Dhambi iliingia humu duniani katika Bustani ya Eden wakati mtu kwa hiari yake alipokataa kumtii Mungu.

   Mungu kwa uwazi alimpa mwanadamu maagizo, lakini shetani aliwaongoza Adamu na Hawa kuona mashaka juu ya Neno la Mungu na wakala tunda toka kwa mti waliokatazwa na Mungu.

   b) Katika Biblia, mwanadamu anapewa maagizo ya mambo anayohitajika kuyafanya ili kumpendeza Mungu.

Kila wakati tunapoamua kutofanya maagizo yake tunatenda dhambi. Dhambi ni kufanya kitu chochote kisichompendeza Mungu.

**3.** **<u>Dhambi ipo katika mawazo yetu</u>.**

**Soma Mathayo 5:27-28**

**Kielezo:** Ndugu wawili walikuwa wakipigana. Baba yao aliwaadhibu kwa kumwamuru kila mmoja wao kuketi katika pembe tofauti ya chumba. Huyo baba aliwaamua wavulana hao wasipigane, lakini hao wavulana walikuwa wakipanga jinsi ya kuumizana. Wavulana hao waliacha kupigana, lakini walikuwa na chuki na kutosameheana – walikuwa bado wanapigana mioyoni mwao.

a) Watu wengi husema kwamba wao hawana dhambi kwa vile hawatendi maovu. Lakini ndani ya mioyo yao kuna chuki, uchungu, tamaa, n.k.

b) Dhambi sio kutomtii Mungu kwa nje tu, bali pia kwa undani wa Neno Lake.

**4.** **<u>Dhambi ipo ndani ya midomo yetu</u>.**

**Soma Mithali 10:19**

Biblia inazungumza mengi kuhusiana na uwezo wa ulimi. Mungu hatufundishi tu nini cha kufanya na kufikiria, bali hutufundisha pia jinsi ya kumfurahisha kwa midomo yetu.

Umbea, uongo, masengenyo, uchonganishi, laana, n.k., haimpendezi Mungu. Yakobo 4:11.

**5.** **<u>Dhambi ipo katika asili ya mwanadamu</u>.**

**Soma Warumi 5:12, 19**

**Kielezo:** Mama alisikitika wakati alipomkuta mtoto wake mdogo wa kikeakijaribu kuiba chakula toka jikoni. Mama huyo alishangaa alikojifunza mtoto huyu kuiba.

a) Sisi sote tumerithi dhambi ya asili kutoka kwa Adamu kwa hiyo dhambi imo katika uzao wetu.

b) Mtoto hahitaji kufundishwa jinsi ya kutenda dhambi – hiyo huja yenyewe. Watoto wetu wamerithi dhambi ya asili kutoka kwetu. Biblia haisemi tu kwamba tunatenda dhambi, bali sisi ni wadhambi.

## C. Wote ni wenye dhambi

**Soma 1 Yohana 1:8**

**1.** Tunapofikiria kuwa dhambi ni nini ni lazima tukubali kwamba wote wametenda dhambi. Hakuna asiyehusika.

**2.** Sote tunahitaji msaada wa Mungu ili tuweze kupambana na dhambi.

## Aya ya kukumbuka

Warumi 3:10-11, 23, *"Hakuna mwenye haki hata mmoja ... hakuna mmoja anayefahamu,hakuna mmoja amtafutaye Mungu ... kwa sababu wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu".*

## Muhtasari wa Mwalimu

1. **Soma Ezekieli 28:12-17 na Isaya 14:12-17.**

   Huu ni unabii unaomhusu shetani. Weka maanani, ni mara ngapi shetani katika kiburi chake alisema (katika Isaya) "nitafanya".

2. **Soma Mwanzo 3:1-6.**

   Weka maanani kifungu cha 1, "Ati, hivi ndivyo alivyosema Mungu?"

3. **Soma Mathayo 4:1-11.**

   Tambua kwamba shetani bado anajaribu kugeuza maana ya Neno la Mungu. Jibu letu kwa maneno ya shetani ni sawa na lile la Yesu: Ni kujua ukweli wa neno la Mungu. Angalia kifungu cha 4, 7, na 10 – Yesu alisema, "Imeandikwa".

# Matokeo ya dhambi

**Somo la 4**

## A. Utangulizi

**Soma Warumi 3:10, 23**

Katika somo lililopita tulijifunza kwamba watu wote ni wenye dhambi.

Warumi 3:23 inatuambia kwamba tumepungukiwa na utukufu wa Mungu. Hebu sote tufikirie maana yake.

## B. Uhusiano wa mwanadamu na Mungu

**Soma 1 Yohana 4:8**

**1.** Katika kifungu hiki tunaona tabia fulani ya Mungu. Mungu ni pendo. Mungu hapendi hivi hivi tu; Yeye mwenyewe ni pendo.

**2.** Kwa kuwa Mungu ni pendo, anahitaji mtu wa kumwonyesha upendo huo. Adamu na Hawa walitimiza hitaji hilo la Mungu katika Bustani ya Eden. Waliufurahia ushirika wa Mungu pamoja na baraka bustanini.

## C. Mungu ni Mungu mtakatifu

**Soma Habakuki 1:13a**

Kifungu hiki chatuambia kitu kingine zaidi kuhusiana na tabia ya Mungu. Yeye ni Mungu mtakatifu asiyeweza kukaa katika dhambi.

## D. Dhambi humtenga mtu na Mungu.

**Soma Isaya 59:2**

**1.** Ushirika ambao mwanadamu aliufurahia akiwa bustanini ulivunjika wakati mwanadamu alipotenda dhambi.

**2.** Tunaweza kusema, "Ikiwa Mungu ni Mungu wa upendo, kwa nini uhusiano huu ulivunjika?" Jibu ni kwamba, Mungu ni Mungu mtakatifu na hawezi kuvumilia dhambi.

**Kielezo:** Ili uweze kufahamu nafasi ya mtu mwenye dhambi mbele za Mungu, hebu fikiria picha ya korongo kubwa. Kwa pembe moja ya korongo unaonekana utukufu wa Mungu, na kwa pembe nyingine ya korongo amesimama mtu mdhambi. Kati ya utukufu wa Mungu na mwanadamu, kuna shimo kubwa (dhambi) ambayo inamtenganisha Mungu na mwanadamu. Kutokana na hayo, binadamu hawezi tena kufurahia baraka za mwenyezi Mungu.

## E. Matokeo ya utengano huu

### 1. **<u>Kifo</u>.**

**Soma Mwanzo 2:17**

**<u>Dhambi huleta mauti kwa mwanadamu kwa njia tatu</u>:**

a) **<u>Mauti ya mwili</u>.**

Dhambi ilileta magonjwa na mauti duniani. Siku Adamu na Hawa walipotenda dhambi, miili yao ya asili ilianza kufa. Mwanzo 5:5.

b) **<u>Mauti ya kiroho</u>.**

**Soma Waefeso 2:1**

i) Maandiko haya yawahusu watu ambao kimwili ni hai lakini wamekufa.

ii) Leo hii, watu wasio na Kristo wamekufa kiroho.

iii) Dhambi humtenga mtu na ushirika wa Mungu. Mtu mwenye dhambi hawezi kuwasiliana na Mungu.

c) **<u>Mauti ya milele</u>.**

**Soma Warumi 6:23**

Kuna wakati ambapo kila mtu anakufa, na mwili wake utakwenda kaburini. Nafsi, yule mtu halisi katika mwili, haendi kaburini bali itaishi milele.

Bila kuwa na Kristo, nafsi ya mtu hetengwa na upendo wa Mungu milele katika jehanamu. Hii ndiyo mauti mbaya kabisa kuliko zote.

### 2. **<u>Hatia</u>.**

**Soma Mwanzo 3:7-10**

a) Adamu na Hawa walikuwa na amani na Mungu bustanini. Kwa sababu ya hatia na aibu ya dhambi yao, baadaye tumewaona wakijificha kwa kumhofu Mungu.

b) Hivi leo watu wengi hawakubali ya kuwa wao ni wenye dhambi, lakini hatia ya dhambi zao inalemea mioyo yao na kuwanyang'anya amani.

### 3. **<u>Masikitiko</u>.**

**Soma Mwanzo 3:14-19**

a) Kabla ya kutenda dhambi, mwanadamu alikuwa huru kutokana na ugomvi na mahitaji yake yote alipatiwa. Baadaye Mungu alisema kwamba mwanadamu atapambana na shetani (kifungu cha 15) na kwa jasho atakula.

b) Leo hii tunaona kwamba dhambi imeleta masikitiko mengi katika maisha ya watu. Hii ni pamoja na madawa ya kulevya, ndoa nyingi kuvunjika, ugomvi, umasikini, uhalifu, n.k.

**4. Giza.**

**Kielezo:** Mtu mmoja alilazimika kusafiri usiku katika nchi ambayo alidhani ina mashimo mengi sana. Kabla ya giza kuingia, mtu huyu aliweza kuiona njia yake kwa urahisi na kukwepa mashimo, lakini giza lilipoingia alijikwaa na kutumbukia mashimoni, akajiumiza.

**Soma Mithali 4:19**

a) Dhambi huleta giza.

b) Bila mwangaza wa uwepo wa Mungu, mwanadamu hujikwaa gizani na hajui njia sahihi ya kuifuata. Hivyo mwanadamu huangukia katika kila aina ya mitego ambayo shetani huitega ili amwumize.

**5. Kifungo.**

**Soma Yohana 8:34**

Dhambi humfanya mwanadamu kuwa mtumwa. Hawezi kufanya anavyotaka, bali huwa kama mtu aliyefungwa minyororo. Yeye ametengwa na uhuru ule utokanao na kumjua Mungu.

## F. Mwanadamu hana kitu cha kufanya ili ajiokoe

**Soma Yeremiah 2:22**

**1.** Akiwa amepotea na kufungwa dhambini, mwanadamu hujaribu njia nyingi za kujinasua kutokana na hali hiyo.

**2.** Watu wengi hudhania kuwa matendo mema, sala, elimu nzuri, dini mbali mbali, kujaribu kuwa mwema, n.k., vitawasaidia. Mithali 14:12.

**Kielezo:** Tunarudi tena kwenye picha yetu ya korongo kubwa la dhambi inayotutenga na Mungu. Watu hujaribu kutumia vitu tulivyoorodhesha hapo juu kujenga daraja la kuvukia korongo. Biblia yaeleza wazi kwamba vitu hivi vyote haviwezi kuondoa utengano huu.

Hakuna kitu ambacho mwanadamu ataweza kufanya ili aurudishe ushirika wake na Mungu. Matendo 4:12.

Juhudi zote za mwanadamu hata ziwe nzuri vipi, haviwezi kumwondolea hatia ya dhambi. Isaya 64:6.

## G. Yesu Kristo ndiye jibu pekee

**Soma Warumi 7:24-25**

**1.** Pamoja na habari zote hizo mbaya, tunaweza kujiuliza ikiwa kuna tumaini lolote kwa mwanadamu.

**2.** Habari njema hupatikana ndani ya Yesu Kristo. Ni damu ya Yesu pekee inayoweza kutuondolea dhambi zetu na kuurudisha ushirika wetu na Mungu.

### Aya ya kukumbuka

Isaya 59:2, *"Lakini maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu; na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone, hataki kusikia".*

### Muhtasari wa Mwalimu

Kumpokea Yesu na nguvu za damu yake ndiyo njia ya pekee ya kuurejesha ushirika wetu na Mungu. (Waefeso 2:13). Zingatia yafuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| **1.** | **Dini mbali mbali:** | Yohana 14:6. Yesu hakusema tu kwamba yeye **ndiye** njia ya kumfikia Mungu. Alisema kwamba Yeye ndiye njia **pekee**. |
| **2.** | **Kusali:** | Yohana 3:1-3. Kwa watu wa dini Yesu alisema, "Ni lazima uzaliwe mara ya pili". |
| **3.** | **Matendo mema:** | Waefeso 2:8-9. Matendo mema bila Kristo hayawezi kutuokoa. |
| **4.** | **Elimu:** | 1 Wakorintho 1:18-21. Elimu yote na hekima ya mwanadamu haiwezi kumpatia uzima wa milele. |
| **5.** | **Kumwamini Mungu:** | Yakobo 2:19-20. Mapepo yanamwamini Yesu, lakini hayajaokoka. |

# Mungu anafanya njia

**Somo la 5**

## A. Utangulizi

**Soma Mithali 8:35-36**

**1.** Katika mafundisho machache ya mwisho tumeona kwamba dhambi ndiyo sababu ya utengano kati ya mwanadamu na Mungu, na matatizo yote ya mwanadamu yametokea kwa sababu ya dhambi.

**2.** Tumejifunza pia kwamba hakuna kitu anachoweza mwanadamu kutenda ili ajiondoe kwenye hali hiyo isiyo na tumaini.

**Kielezo:** Kikundi fulani cha watu waliishi kando kando ya mto wa ajabu utoao maji ya uzima. Siku moja, mwamba mkubwa sana ulitumbukia ndani ya mto huo kilometa chache kwa upande wa juu. Tukio hilo lilifanya mto ubadili mwelekeo wake. Watu wakawa hawana maji ya kunywa na ya kuogea. Mimea ikaanza kukauka na kufa kwa kukosa maji. Baadaye pia watu nao wakaanza kufa. Watu walijaribu kwa bidii kurekebisha hali ya mahali walipokuwa. Waliweka mbolea mashambani na kupalilia mimea, na kupanda mengine zaidi. Lakini hayo yote hayakusaidia kubadilisha hali yao. Pasipokuwa na yale maji yatoayo uzima, watu kijijini walikuwa dhaifu, wakawa wagonjwa, na wakaendelea kufa. Watu hao walihitajika kutafuta kiini hasa ya tatizo lao. Walihitajika kupata msaada wa kuwawezesha kuondosha mwamba, ili maji yale yatoayo uzima yaendelee kububujika tena.

**3.** Dhambi ndiyo kiini cha matatizo ya wanadamu. Katika masomo haya yafuatayo tutaona jinsi Mungu alivyoshughulikia kiini hiki cha dhambi na kutupatia uzima.

## B. Mungu siku zote hupanga

**Soma 1 Petro 1:18-20**

**1.** Haikuwa mpango wa Mungu kwa dhambi, magonjwa na taabu kuwapata wanadamu. Mungu atupendaye hututakia mambo yeale mazuri kabisa.

Lakini ili upendo uwe wa kweli, ni lazima mmoja apewe uchaguzi, ama huo hautakuwa upendo kabisa. Mungu alimpa mwanadamu uhuru. Mwanadamu alipewa uchaguzi ampende Mungu lakini yeye alichagua kwenda njia zake.

**2.** Mungu kwa ufahamu wake aliliona anguko la mwanadamu na katika upendo wake alifanya mpango ili mwanadamu arejeshwe.

Siku nyingi sana kabla dunia haijaumbwa, Mungu baba alipanga kwamba Yesu Kristo atakufa msalabani mwa Kalivari kwa ajili ya dhambi za wanadamu. Ni upendo mkuu namna gani huu alionao Mungu, kumtoa mwanawe pekee ili sisi tupate kusamehewa. 1 Yohana 4:10.

## C. Mifereji ya damu katika Agano la Kale

Mafunzo ya Mungu katika agano la kale yaonyesha kwamba ni kwa njia ya damu tu mwanadamu aweza kutakaswa dhambi na kuurejesha uhusiano wake na Mungu.

### 1. <u>Adamu na Hawa</u>.

**Soma Mwanzo 3:21**

Muda mfupi tu baada ya kutenda dhambi, Mungu aliua wanyama wawili kisha akawafunika Adamu na Hawa kwa ngozi ya wanyama.

Alitaka kutuonyesha kitu tokea mwanzo.Wakati Adamu na Hawa wamesimama damu ikidondoka toka ngozi za wanyama, Mungu alikuwa akisema, “ni damu tu itakayofunika dhambi zenu zote”.

Hata kabla ya Kristo kufa msalabani Mungu alikuwa akiiona damu ya Yesu itakayofunika dhambi zote.

### 2. <u>Kaini na Abel</u>.

**Soma Mwanzo 4:3-5**

Haionekani kama ni haki kwa sadaka ya Kaini kukataliwa. Kaini alifanya kazi kwa bidii na akaleta sadaka nzuri.

Lakini Mungu alitaka kuweka wazi kwamba matendo mema na makusudio mema hayatoshi kumaliza dhambi.

### 3. <u>WaIsraeli walikombolewa kutoka utumwani na mauti</u>.

**Soma Kutoka 12:1-14**

Vyura, majipu, tufani, nzige, n.k. .... havikuweza kuwakomboa waIsraeli toka utumwani. Ilikuwa damu ya kondoo asiye na dhambi iliyowapatia uhuru.

Pasaka ilikuwa njia ya Mungu ya kutuonyesha damu ya Yesu Kristo kuwa ndiyo itakayotukomboa kutokana na kifungo cha dhambi na mauti.

### 4. <u>Sadaka za damu</u>.

**Soma Mambo ya Walawi 1:1-5**

a) Njia ya kufikia katika uwepo wa Mungu katika Hema ya Agano la Kale ni kwa kutoa sadaka ya damu. Wakati wote wa Agano la Kale ilichuruzika mifereji ya damu.

b) Hakukuwa na nguvu ya siri katika damu ya madume, kondoo na mbuzi. Mungu aliruhusu hii ili iwe ishara ambayo itavuta nguvu zake kwa damu ya Kristo.

Utambue kwamba sadaka haikutakiwa iwe na mawaa, ikionyesha sadaka ya Kristo ambaye hakuwa na dhambi.

## D. Sadaka ya mwisho

**Soma Waebrania 10:10-14**

**1.** Sadaka zote za damu wakati wa Agano la Kale zilikuwa zikituelekeza kwa damu ya Yesu Kristo – mwana kondoo asiyekuwa na doa ambayo alichukua dhambi za ulimwengu. Yohana 1:29.

**2.** Kwa damu yake tumefanywa kuwa watakatifu milele. Sadaka yake ilitolewa mara moja kwa wote. Ni ya mwisho na kwa kila mtu, kwa hiyo umwagaji mwingine wa damu haina umuhimu.

## E. Damu imefanya njia

**Soma Waefeso 2:13**

**1.** Kupitia damu ya Yesu ile dhambi iliyotutenga na Mungu imeshughulikiwa. Kilichokuwa hakiwezekani kwa mwanadamu, Mungu alikifanya kwa kifo cha Mwanawe.

**2.** Sasa tuko huru kuja mbele za Mungu na kuufurahia ushirika naye milele.

Ni Mungu wa ajabu! Ni utoaji mkubwa namna gani!

### Aya ya kukumbuka

Waebrania 10:10, *"Katika mapenzi hayo tumepata utakaso, kwa kutolewa mwili wa Kristo mara moja tu"*.

### Muhtasari wa Mwalimu

Hebu fikiria damu ya Yesu Kristo iliyomwagika msalabani.

| | | |
|---|---|---|
| **1.** | Ilitutakasa | Mambo ya Walawi 17:11. |
| **2.** | Ilitusafisha | 1 Yohana 1:7. |
| **3.** | Inamshinda shetani | Ufunuo 12:11. |
| **4.** | Ilitununua | Matendo 20:28. |
| **5.** | Ilitukomboa | Wakolosai 1:13-14. |
| **6.** | Ilitupa haki | Warumi 5:8-9. |
| **7.** | Iliosha dhamiri zetu | Waebrania 9:14. |
| **8.** | Ilitupatia msamaha | Mathayo 26:27-28. |
| **9.** | Ilituweka huru | Ufunuo 1:4-5. |

# Yesu yu hai

**Somo la 6**

## A. Utangulizi

**Soma Wakorintho 15:1-8**

Katika somo lililopita tulijifunza kwamba Yesu alikufa kwa ajili yetu. Ni jambo la jabu kujua kwamba kifo cha Yesu kimetusafisha dhambi zetu. Lakini habari hii njema haitakamilika tukiacha kukiri kwamba Yesu amefufuka kutoka kwa wafu. Habari njema ni kwamba **Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zetu**, **akazikwa na** siku ya tatu **akafufuka** kutoka kaburini.

Katika historia viongozi wengi wa dini walidai kuwa wameleta wokovu. Watu wote hao walikufa na miili yao imebakia makaburini.

Kaburi lile ambamo alizikwa Yesu liko tupu. Kristo alifufuka! Yeye yu hai! Yohana 20:3-9. Ukweli huu umeshuhudiwa na wengi. Yesu alijionyesha kwa zaidi ya watu mia tano kwa wakati mmoja.

## B. Mpango wa Mungu ulitimia

**Soma Matendo 26:22-23**

**1.** Siyo Wayahudi, ama Warumi, au shetani aliyemlazimisha Mwana wa Mungu kwenda msalabani. Yohana 19:11.

Yesu alijitoa kwa hiari yake mwenyewe. Mathayo 20:28.

**2.** Yesu aliwatangazia wanafunzi wake kuwa atakufa na kufufuka tena. Mathayo 16:21.

**3.** Siyo damu ya Agano la Kale tu iliyomwelekeza Kristo msalabani, bali Mungu pia alizungumza kupitia mitume wake akiutangaza mpango huo. Kwa wakati uliokubalika Yesu alilitimiza Neno la Mungu.

Kristo alikubali kukabiliana na kifo cha kutisha kwa sababu alijua uwezo wa kifo na ufufuo wake utatufanyia nini. Waebrania 12:2.

## C. Nguvu za Msalaba

**1.** **Tutaweza kumfahamu.**

**Soma Yohana 3:3-8**

a) Tunamtumikia mwokozi aliye hai. Yeye yu hai na anataka tumjue. Huwezi kumfahamu mtu aliyekufa. Kwa kuwa Yesu yu hai, tunaweza kumfahamu kibinafsi.

b) Kitu cha asili hakiwezi kuwasiliana na kitu cha kiroho. Roho yetu iliyokufa ndani mwetu imekuwa hai ili iwasiliane na Mungu. Biblia huiita hali hii “kuzaliwa mara ya pili”. Roho wa Kristo ndani mwetu huleta nguvu ya ufufuo kuzifanya roho zetu kuwa hai.

**2. <u>Tuna amani</u>.**

**Soma Warumi 5:1-2**

a) Watu wasiokuwa na Kristo hutembea chini ya mzigo wa hatia. Hawajui kinachowasu mbua lakini hatia ya dhambi inalemea mioyo yao.

b) Damu ya Yesu iliondoa dhambi na hatia iliyotutenga na Mungu. Dhambi zetu zimesamehewa na Mungu asema kwamba hazikumbuki tena dhambi zetu. Isaya 43:25. Sasa tunaweza kufurahia amani rohoni, na kuufurahiuhusiano wetu na Mungu ambao ilikuwa kusudi lake toka mwanzoni.

Ni uhuru ulioje unaopatikana kwa kumpokea Kristo! Mzigo wa dhambi unaondolewa.

**3. <u>Tunaridhika</u>.**

**Soma Yohana 4:13-14**

a) Bila Kristo kunakuwa na utupu katika mioyo ya watu.

Watu hujaribu kila kitu ili kuujaza huo utupu. Inaweza kuwa kazi, pombe, madawa,mali, n.k. ... lakini hakuna hata kimoja kinachotosheleza. Kwa hiyo watu hujaribu kufanya kila kitu ili kujaza huo utupu.

b) Utupu huo katika moyo wa binadamu unaweza kujazwa tu kwa uwepo wa Yesu Kristo. Yohana 17:26.

Tunapompokea Kristo, chemichemi ya maji ya uzima hutokea moyoni kutosheleza kila hitaji ya moyo.

**4. <u>Tunawekwa huru kutokana na nguvu ya mauti</u>.**

**Soma Waebrania 2:14-15**

a) Yesu alishinda nguvu ya mauti alipofufuka kutoka kwa wafu. Matendo 2:4.

b) Tukiwa na Kristo maishani mwetu, mauti haina nguvu tena juu yetu. Wakolosai 3:3-4.

c) Hofu kubwa sana ya mwanadamu ni kifo. Tunapofikiria ubaya wa moto wa jehanamu, wakati mwingine inafanya mauti iogopwe.

Lakini katika Kristo tunawekwa huru na hofu hii ya kifo na jehanamu. Mungu alituahidi sisi uzima wa milele pamoja naye. Yohana 5:24.

5. **<u>Tumewekwa huru na kongwa la shetani</u>.**

**Soma Wakolosai 2:15**

a) Shetani alidhani kuwa amemshinda Kristo pale msalabani. Lakini Yesu alipofufuka kutoka kwa wafu, aliushangilia ushindi wake kwa shetani. 1 Yohana 3:8.

b) Tunapokuwa ndani ya Kristo tumefufuliwa pamoja naye. Shetani hana mamlaka tena juu yetu. Tunapokuwa na Kristo, tunashangilia dhidi ya kazi za shetani.

Hatuhitaji tena kuogopa nguvu zozote za giza za shetani. Waefeso 6:12.

6. **<u>Tunapokea nguvu za Mungu za uponyaji</u>.**

**Soma 1 Petro 2:24-25**

a) Mungu hakutuumba kwa ajili ya magonjwa na mateso. Alituumba tuwe wazima kimwili, nafsi na roho.

b) Damu ya Yesu iliyomwagika msalabani iliwezesha nguvu za Mungu za uponyaji zipatikane kwa ajili yetu.

Watu wengi ambao akili zao ziliharibiwa na madawa ya kulevya na pombe waliponywa akili zao kabisa walipomjia Kristo. Wengine waliotumika vibaya waliporudi kwa Kristo waliponywa hisia zao za nafsi. Kuna shuhuda nyingi za wale waliompokea Kristo na kupokea miujiza ya uponyaji katika miili yao.

Nguvu ya Mungu ya ufufuo ina uwezo wa kugusa kila sehemu ya utu wetu na kila eneo la maisha yetu.

7. **<u>Kutupatia sisi uzima tele</u>.**

**Soma Yohana 10:10**

a) Yesu alikufa na kisha akafufuka tena ili atupatie uzima. Maisha tele sio baada ya kufa tu, bali ni kuanzia hapa, sasa.

b) Nguvu sawa na ile iliyomfufua Kristo kutoka kwa wafu imo kwetu pia. Waefeso 1:19-20.

Nguvu hizi za ufufuo zifanyazo kazi ndani mwetu zitatuwezesha kuishi maisha ya ushindi. Kwa nguvu zake za ufufuo zifanyazo kazi ndani yetu Yeye hutuwezesha kufanya vitu vya kumpendeza Mungu.

Tumepewa haki ya kuifuurahia uzima tele na tukitembea na Mungu.

## Aya ya kukumbuka

Yohana 14:6, *"Yesu akajibu, 'Mimi ndimi njia na kweli na uzima. Mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi"*.

## Muhtasari wa Mwalimu

Mambo mengine zaidi juu ya msalaba:

| | | |
|---|---|---|
| a) | Inafunua upendo wa Mungu kwetu. | 1 Yohana 4:10. |
| b) | Tumeahidiwa moyo mpya. | Ezekieli 11:19-20. |
| c) | Kwa imani. | Warumi 4:3. |
| d) | Siyo kwa kutii sheria. | Matendo 13:39. |
| e) | Siyo kwa kustahili. | Warumi 4:4-5. |
| f) | Ni kwa neema ya Mungu tu. | Warumi 3:24. |
| g) | Mungu hupokea utukufu wote. | Warumi 11:30-36. |
| h) | Unatuokoa na ghadhabu ya Mungu. | Warumi 5:9. |
| i) | Dhambi zetu zinafunikwa kwa damu ya Yesu. | Warumi 4:7-8. |

# Kitu gani lazima tufanye

**Somo la 7**

## A. Utangulizi

**Soma Kutoka 12:13**

1. Tumeona kazi ya nguvu za msalaba. Kristo kwa damu yake aliwakomboa wanadamu wote na kufungua njia ya kuishi kwa uhusiano ulio hai pamoja na Mungu. Waebrania 10:19-22.

2. Tumeona picha ya nguvu katika Kutoka 12 ambapo watu wa Mungu walikombolewa utumwani. Lakini waliookoka ni wale tu waliopaka damu ya mwana kondoo katika miimo ya milango ya nyumba zao.

3. Tunaweza kufahamu yote kuhusu damu ya Kristo na nguvu za ufufuo wake. Hata hivyo, tusipotumia damu hiyo mioyoni mwetu hatutakombolewa na kutokana na utumwa wa dhambi.

   Wokovu kupitia damu ya Kristo imewekwa kama zawadi ya ajabu ya bure kwa mtu yeyote atakayeipokea na kufanyia kazi maishani mwake.

## B. Tumia damu

**Soma 1 Yohana 1:8-9**

1. Ili kumjia Mungu, ni lazima dhambi iliyotutenga naye ishughulikiwe kwanza. Ni damu ya Yesu tu iwezayo kuondoa dhambi hiyo.

2. Tunatumia damu ya Kristo wakati tunapomtubia Mungu kwamba sisi tu wenye dhambi na kukiri kwamba tunahitaji msaada wake.

3. Tunapofanya hivyo, Yeye huahidi kutusamehe dhambi zetu na kutakasa mioyo yetu kutokana na dhambi zetu.

## C. Toba ya kweli inayohitajika

**Soma Matendo 3:19**

1. Mungu katika Neno lake, anatupa changamoto ili tutubu dhambi zetu.

2. Toba ya kweli ni zaidi ya kukiri dhambi zetu kwa Mungu. Neno la Kiyunani "metanoia" lilitumika katika Agano Jipya kumaanisha uamuzi toka moyoni wa kufuata mwelekeo mpya.

   Kwa hiyo toba siyo tendo tu la kukiri kwa vinywa vyetu kwamba sisi ni wadhambi, bali ni kutubu dhambi zetu kutoka ndani ya mioyo yetu, Matendo 2:37. Na kutoka ndani ya mioyo yetu tunafanya uamuzi wa kugeuka kuacha njia ya dhambi na kutembea ndani ya mapenzi ya Mungu. Mithali 28:13.

## D. Kwa imani

**Soma Warumi 10:9-10**

1. Wokovu hauwezi kupatikana kwa kujaribu kumfurahisha Mungu. Ni kwa neema tu. Waefeso 2:8-9.

   Hatutaweza kamwe kuwa wazuri wa kutosha ndani mwetu, na hakuna gharama tutakayoweza kulipa kwa ajili ya wokovu wetu. Kristo alilipa yote kwa damu yake msalabani.

2. Wokovu waweza kupatikana tu kama kipawa cha bure kutoka kwa Mungu kwanjia ya imani. Warumi 6:23.

   Imani ni kuamini kutoka mioyoni mwetu yale yote Mungu aliyosema yametimizwa msalabani ni kweli, na kuwa ni kwaajili yetu. Sio tu kwamba Yesu alikufa kwa ajili yetu bali, “kwamba Mungu alimfufua kutoka kwa wafu”, kwa ajili yetu.

   Kwa mayo twaamini na kwa vinywa twanena na kutia muhuri wokovu wa Mungu kwa maisha yetu.

## E. Mpokee Kristo

**Soma Ufunuo 3:20**

1. Yesu hawezi kujilazimisha ndani ya maisha ya mtu. Anataka jibu toka moyoni.

   Leo hii Kristo kwa upole anabisha mlangoni mwa mioyo ya watu. Anampa kila mtu changamoto amfungulie mlango wa moyo wake na kumkaribisha ndani. Kristo aliahidi kwamba ataingia na kufanya ushirika nasi.

   Ni ahadi ya ajabu! Mungu aliyetuumba kuwa na ushirika nasi, na kuishi ndani mwetu. 2 Wakorintho 13:5.

2. Kwa nguvu zake zinazofanya kazi ndani yetu anaanza kutubadilisha.

   Watu wengi walijaribu kuwa wema ili wamwendee Mungu, lakini Mungu anasema, "Njooni kwangu kupitia damu ya Kristo na nitatumia nguvu zangu takatifu ndani yako".

   **Kielezo:** Mtu mmoja alihudhuria kanisani maisha yake yote, na sasa ni mzee. Yeye husoma Biblia na husali. Alifahamu habari za Yesu na nguvu za msalaba, lakini katika maisha yake yote alikazana ili kumfurahisha Mungu na bado hakuwa na uhakika kuhusu wokovu wake. Siku moja alisikia mtu akiihubiri injili. Alipopewa changamoto, huyo mtu alitubu dhambi ya kujaribu kuishi maisha mazuri kwa nguvu zake na akamwomba Yesu aingie ndani ya moyo wake. Mara mtu huyo alipata furaha na amani moyoni mwake na uhakika wa wokovu wake ambao siku zote alikuwa akiutafuta.

## F. Maombi ya kumpokea

Hapa kuna sala iliyopendekezwa kwa ajili ya kumpokea Yesu. Sala hii siyo sheria maalum, lakini tunachohitaji kuomba lazima itoke moyoni.
Sala hii lazima iwe na maneno yafuatayo:

**Baba nakuja kwako katika jina la Yesu.**
**Naungama dhambi zangu kwako na ninakiri kuhitaji wokovu wako.**
**Naamini kwamba ulikufa msalabani kwa ajili yangu na ukafufuka tena kutoka kwa wafu.**
**Naomba unisamehe na kunitakasa kutokana na matendo yote maovu.**
**Nina kua lika uingie ndani mwangu na kuwa Bwana wa maisha yangu.**
**Kwa imani katika nguvu zako zifanyazo kazi ndani yangu nakushukuru Bwana kwamba nitaishi maisha ya kukupendeza wewe.**

Kumbuka kuwa wokovu wetu hau tegemei kujisikia kwetu bali ni kwa imani juu ya yale Mungu amesema ata ya fanya kupitia neno Lake. 2 Petro 1:4.

Kama umeomba maombi haya, basi Mungu amekusamehe, Kristo amekuja moyoni mwako, wewe ni mwana wa Mungu na Yesu ni Bwana wa maisha yako. Mungu ni kweli kwenye ahade Zake. 2 Korintho 1:20.

## G. Mruhusu Yesu awe Bwana wa maisha yako

**Soma Wakolosai 2:6**

**1.** Kumkiri Yesu kama Bwana siyo maneno matupu tu. Warumi 10:9-10. Tunakiri nguvu za msalaba – kwamba Yesu ni Bwana wa wote. Wafilipi 2:8-11.

**2.** Maisha tunayoishi ili kujifurahisha wenyewe yanatuongoza kwenye utupu. Mathayo 10:39. Tunapompokea Yesu tunahitaji kumruhusu Yeye awe Bwana wa maisha yetu.

Tujitoe awe Bwana tokea mwanzoni na kumwuliza Kristo ayatawale maisha yetu. Luka 14:27. Maisha mazuri unayoweza kuishi ni kwa kufanya mapenzi yake.

### Aya ya kukumbuka

Warumi 10:9, *"Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka".*

## Muhtasari wa Mwalimu

Ushauri uliopendekezwa kwa wale waliompa Kristo maisha yao.
Elezea ulazima:

**1.** Kuanza kwa kuendelea kushuhudia wengine habari za Kristo. Mathayo 10:32.

**2.** Kupata Biblia na kuisoma kila siku, Mathayo 4:4. Watie moyo wasome vitabu vya injili kwanza kabla ya kusoma sehemu zingine za Biblia.

**3.** Kuujenga uhusiano wetu na Mungu kwa njia ya maombi kila siku. Yohana 16:23-24.

**4.** Kuhudhuria kanisani na kushirikiana na wakristo wengine. Waebrania 10:25.

**5.** Kubatizwa mapema iwezekanavyo. Matendo 2:38.

**6.** Kujazwa na Roho Mtakatifu. Luka 11:11-13.

# Sisi ni viumbe vipya

**Somo la 8**

## A. Utangulizi

**Soma 2 Wakorintho 5:17**

**Kielezo:** Kuzaliwa kwetu mara ya pili inatufanya tuwe viumbe vipya. Ni kama kiwavi mwenye sura mbaya anapobadilishwa kutoka kiwavi na kufanywa kuwa kipepeo mzuri ambaye yu huru kunyosha mbawa zake na kuruka.

Wakristo wengi hawajitambui jinsi wanavyopendeza mbele za Mungu na uhuru walionao sasa katika Kristo, na kwa kutotambua hivyo huendelea kutambaa kama viwavi.

## B. Hebu tufikirie ni kwa njia zipi tumekuwa viumbe vipya ndani ya Kristo

**1. Moyo mpya.**

**Soma 2 Wakorintho 5:21**

a) Kuwa mwenye haki ni kuwa na haki mbele za Mungu, kutokuwa na dhambi. Kwa sababu ya damu ya Yesu, Mungu atuangaliapo huona mioyo mipya.

b) Hii haimaanishi kwamba hatuwezi tukatenda dhambi. 1 Yohana 1:8.

Tunapotenda dhambi tunahitaji kutubu na damu ya Yesu itafanya mioyo yetu kuwa safi siku kwa siku. 1 Yohana 1:9.

c) Shetani atajaribu kutukumbusha dhambi zetu za zamani, ili kujaribu kutufanya tuinamishe vichwa vyetu kwa hatia na kukimbia kutoka kwenye uwepo wa Mungu kama Adamu na Hawa.

Lazima tukumbuke uwezo wa damu, kuinua vichwa vyetu juu na kutembea na uhusiano wa karibu na Mungu. Isaya 43:25.

**2. Uhusiano mpya.**

**Soma Yohana 1:12**

a) Siyo kila mtu dunia ni mtoto wa Mungu. Watu wote waliumbwa ili wawe watoto wake lakini ni wale tu waliompokea Kristo ndio watoto wa Mungu.

b) Watoto wa asili wanao upendeleo kwa baba yao wa asili kuliko watoto wengine. Hufurahia ushirika wake, ulinzi, kupatiwa mahitaji yao, n.k.

c) Sasa Mungu ni Baba yetu. Anataka tuufurahie upendeleo wa kuwa watoto wake, akitupatia mahitaji yetu yote. Wewe ni mtu wa jamii ya Mungu na mwanachama wa nyumba ya Mungu.

3. **Nafasi mpya.**

**Soma 1 Wakorintho 12:12, 27**

a) Kama wakristo kila mmoja wetu hufanyika kiungo cha mwili wa kiroho wa Mungu duniani.

b) Kristo huuangali mwili wake, yaani Kanisa kuwa wa muhimu sana. Wewe nimwakilishi wa kimwili wa Kristo hapa duniani. Yeyote anayekugusa wewe anamgusa Kristo. Matendo 9:1-5. Huu ni upendeleo mkubwa, na pia ni wajibu mkuu.

c) Kristo ndiye kichwa cha Mwili wake hapa duniani. Wakolosai 1:18.

Kama vile vichwa vyenu vya asili vinavyoongoza miili yenu, mumtazamie Kristo awaongoze ninyi sasa kama viungo vya mwili wake.

**Kielezo:** Mtu mmoja alijikwaa mguu wake kwenye mwamba na kuvunjika kidole chake kidogo; kimojawapo cha viungo vidogo vya mwili wake. Kichwa cha mtu huyo mara moja kilielekeza kila kitu kwenye kukisaidia na kuilinda kiungo hicho kinliachoumia.

Unaona kichwa chetu cha asili kinahusika kabisa kwenye viungo vya miili yetu ya asili. Haijalishi ni vidogo namna gani, viungo vya miili yetu ya asili ni muhimu sana kwetu.

Kwa njia hiyo hiyo Kristo naye alijitoa kwenu. Ninyi ni viungo vya mwili wake na ninyi ni wa muhimu sana Kwake.

4. **Mamlaka mapya.**

**Soma Luka 10:19**

a) Yesu akasema, “Nimewapa **ninyi** mamlaka ... juu ya nguvu **zote** za adui”.

Kristo alimshinda shetani pale msalabani na sasa ameketi kwenye mamlaka juu ya mamlaka yote na nguvu. Waefeso 1:18-23.

Mahali pale palipo kichwa, mwili pia upo pale. Waefeso 2:6. Tumeketi pamoja na Kristo katika mamlaka juu ya nguvu zote za giza.

b) Shetani hujaribu kuwadanganya wakristo ili waamini ya kuwa yeye shetani ana nguvu kuliko wao. 1 Petro 5:8.

Tunahitaji kumpinga na kumwambia aende zake Katika Jina la Yesu. Yakobo 4:7.

**Kielezo:** Kijana mmoja aliyempokea Kristo alikuwa bado akiamshwa usiku na mapepo waliyemtisha na kumtia hofu nyingi. Huyo kijana alimsikia mhubiri akifundisha kutoka Luka 10:9 kuhusu mamlaka ambayo waaminio wanayo ndani ya Kristo juu ya shetani. Mapepo hayo yalipokuja usiku huo, badala ya

kuogopa yule kijana aliyapinga mapepo hayo na kuwaamuru wakimbie. Mapepo yalitoroka na kijana akalala kwa amani.

**5. <u>Ufunuo mpya</u>.**

**Soma Ufunuo 3:20**

a) Tunapotubu na kumwomba Yesu awe Bwana wa maisha yetu, Roho wake Mtakatifu huja na kukaa ndani mwetu.

Kristo anapoishi ndani mwetu hutufunulia jinsi ya kuishi maisha mapya yampendezayo Mungu.

b) Nguvu za Roho Mtakatifu zilizomo ndani mwetu ni zile zile nguvu zilizomfufua Kristo kutoka kwa wafu. Ni nguvu hiyo hiyo iliyoiumba dunia. Ni nguvu za Mungu. Warumi 8:9-11. Kwa nguvu hizo tunaweza kufanya kitu chochote ambacho Mungu anataka tukifanye. Wafilipi 4:13.

c) Tunaweza kumwamini Mungu. Tunapojitoa kwake tunaweza kupumzika ndani yake. Mungu ataimaliza kazi yake kupitia kwetu. Atatuongoza katika matembezi yetu mapya ndani yake.

## Aya ya kukumbuka

2 Wakorintho 5:17, *"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; yakale yamepita; tazama, yamekuwa mapya"*.

## Muhtasari wa Mwalimu

**Soma Waefeso 1:17-20**

Omba sala hii kwa ajili yako mwenyewe na kwa ajili ya watu utakaowafundisha. Ni kitu kingine kuijua kweli katika nia zetu, lakini ili kutembea kwa ushindi tunahitaji kuombea ufunuo wa kiroho ndani ya mioyo yetu kwa nafasi tuliyonayo ndani ya Kristo. Mwombe Roho Mtakatifu agawe ufunuo huo katika mioyo ya watu unaowafundisha.